# Maandiko Yanasema Nini Kuhusu Madhehebu?

(Sehemu ya Kwanza)

Kuna madhehebu maelfu duniani siku hizi, lakini wazo hili (la madhehebu) siyo la kimaandiko lakini watu bado wanapenda madhehebu kumbe wazo hili halikutoka kwa Mungu.

I**. Biblia inafundisha kuna kanisa moja.**

A. Efe. 4:4-6; Kuna miili mingapi? ________________________
B. Rum. 12:4-5; Kuna miili mingapi? _______________________
C. 1 Kor. 12:12-13; Kuna miili mingapi? ____________________

**II. Kwa nini madhehebu yanatokea? Soma 1 Kor. 1:10-13.**

A. Katika mstari wa 10 tunaona kwamba Paulo aliongea kuhusu mambo manne.
   1. Kwanza alisema, "Nyote mnene _______________."
   2. Tena alisema, "Pasiwe kwenu ________________."
   3. Halafu akasema, "Bali mhitimu katika nia ________________."
   4. Na alimaliza kwa kusema, "Bali mhitimu katika...........shauri ________________."
   5. Lakini tuangalie dini ya Yesu Kristo leo. Hatuongei mamoja, kuna faraka kila sehemu, na nia moja pamoja na shauri moja ni kitu kigeni sana kwa ulimwengu wa leo.
   6. Ndio maana Paulo aliuliza katika mst. 13, "Je, Kristo amegawanyika?"
   7. Kwa sababu Kristo na mafundisho yake ni kitu kimoja. Na kama tunataka kuenda mbinguni pamoja na Baba basi tunahitaji tuwe na umoja kama Yesu na Baba yake walivyo na mmoja.

B. Yesu aliomba katika Yohana 17:20-23, kwamba tusiwe na faraka lakini tuwe na moja, kupitia mafundisho ya mitume, yaani maandiko matakatifu.

C. Kwa nini madhehebu yapo?
   1. 1 Kor. 1:11, Kwa sababu ya ________________.
   2. 2 Tim. 4:3-4.
   3. Kwa hiyo watu wanatamani kitu fulani. Kwa hiyo wanaleta fitina na wanatafuta walimu wauongo kwa sababu wana masikio ya ___________________.
   4. Lakini mwisho wao ni nini? Tuangalie Mat. 15:13-14, "Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni _______________."
   5. Kwa ufupi madhehebu yametokeo kwa sababu watu wameacha ukweli. Na wameaacha ukweli kwa sababu nyingi tu. Labda ni fitina, labda wanataka njia rahisi, labda wanapenda kumfuata mwanadamu tu. Bila kujali, Mungu kama hajapanda na mtu

      mwingine amepanda basi alaaniwe, Gal. 1:6-9.

D. Swali: Kama umechukua Biblia tu, na ulianza kusoma na kufuata Biblia kama ilivyoandikwa. Je! Utapata wapi majina ya Moravia, Luteri, Katoliki, Kanisa la Sabato? Majina yale hawapo! Sasa kama majina yale hayapo, je! Mafundisho yao yapo au mafundisho yao yametoka vitabu vyao? Na kama mafundisho yao yametoka vitabu vyao inamaana Mungu hakupanda.

Kwa hiyo Mungu ata??????